JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, WAKATI WA KUWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

Mhe. Samia Suluhu Hassan (Mb.),
Waziri wa Nchi, Muungano

Mhe. Dkt. Binilith Satano Mahenge (Mb.),
Waziri wa Nchi, Mazingira

I. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2013/14; na malengo kwa mwaka wa fedha 2014/15, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/15.

2. ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya kuwasilisha napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi kilichopita, na ambao wamewezesha kuandaa mipango ya mwaka wa fedha 2014/15 na kustawisha hoja ambayo naiwasilisha katika Hotuba hii. Aidha, nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wa Kamati za Kudumu za Bunge za Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa **James Daudi Lembeli (Mb.)** na ile ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa **William Mganga Ngeleja (Mb.)** kwa kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/15. Vilevile, natoa shukrani kwa Mheshimiwa Mchungaji **Israel Natse (Mb.)** (Mazingira) na Mheshimiwa **Asaa Othman Hamad (Mb.)** (Muungano) Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano na michango yao katika kuboresha Hoja hii.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa **Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kunipa dhamana ya kusimamia masuala ya Muungano; na pia kuwateua Mheshimiwa **Dkt. Binilith Satano Mahenge (Mb.),** kuwa Waziri mwenye dhamana ya kusimamia Mazingira; na Mheshimiwa **Ummy Ally Mwalimu (Mb.),** kuwa Naibu Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Nawashukuru sana Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano na utendaji wao thabiti na makini, katika kutekeleza majukumu ya Ofisi. Aidha, natoa shukrani zangu za pekee kwa Mheshimiwa **Dkt. Therezia Luoga Huvisa (Mb.),** kwa ushirikiano wa dhati alionipa katika kipindi cha miaka mitatu **(3)** tulipokuwa pamoja Ofisini.

4. ***Mheshimiwa Spika***, natumia fursa hii kuwashukuru **Bw. Sazi Bundala Salula** - Katibu Mkuu, **Mhandisi Angelina Elias Madete** - Naibu Katibu Mkuu**, Mhandisi Bonaventure Thobias Baya** - Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**,** Wakuu wa Idara

na Vitengo na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

5. ***Mheshimiwa Spika****,* kazi nzuri iliyofanywa na wote niliowashukuru hapo juu isingewezekana bila ya uongozi thabiti wa **Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo anayotupa katika kusimamia masuala ya Muungano na kuhifadhi Mazingira.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa ndugu, marafiki na wananchi, kwa vifo vya Mheshimiwa **Dkt. William Augustao Mgimwa** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Waziri wa Fedha na Mheshimiwa **Said Ramadhani Bwanamdogo** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze. Aidha, natoa pole za dhati kwa wananchi kwa ujumla kwa kuwapoteza ndugu zao na mali kutokana na ajali za barabarani na maafa ya mafuriko yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Vifo na majanga haya ni pigo kubwa kwa ustawi wa uchumi wa nchi yetu. Tutawakumbuka kwa juhudi zao, na tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii sasa kuwapongeza Mheshimiwa **Geofrey William Mgimwa** Mbunge mpya wa Jimbo la Kalenga na Mheshimiwa **Ridhiwani Jakaya Kikwete** Mbunge mpya wa Jimbo la Chalinze kwa kuchaguliwa na wananchi ili kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu.

8. ***Mheshimiwa Spika***, nawashukuru na kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni, ambazo zimetoa tathmini ya utekelezaji wa jumla katika masuala ya mipango na uchumi; utumishi na utendaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/14 na malengo na mwelekeo kwa mwaka wa fedha 2014/15. Aidha, niwatakie Mawaziri wote watakaofuata kila jema na ufanisi katika kazi hii inayotukabili.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kusema hayo napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14 na malengo kwa mwaka wa fedha 2014/15.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano 2010 - 2015; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2010 - 2015; Malengo ya Maendeleo ya Milenia; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II); Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997; na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191.

II. MASUALA YA MUUNGANO

UTEKELEZAJI WA MAELEKEZO YA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 – 2015 NA MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/14 NA MALENGO KWA MWAKA 2014/15

11. ***Mheshimiwa Spika***, tarehe 26 Aprili, 2014, Muungano wetu umetimiza miaka **50** tangu kuasisiwa kwake. Katika kipindi hicho, sote tumeshuhudia wananchi ndani ya nchi yetu wakipata fursa za kuishi kwa amani na kufanya shughuli za kimaendeleo popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hali hii, inathibitisha kauli isemayo **Utanzania wetu ni Muungano wetu, hatuna budi kuulinda, kuuimarisha na kuudumisha.**

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Hotuba ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2013/14, Ofisi ya Makamu wa Rais iliahidi mambo kadhaa ambayo utekelezaji wake umeendana na maagizo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015 kama yalivyoagizwa kwenye Ibara ya **184.** Uhalisia wa utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Kuratibu Uboreshaji wa Sheria na Kanuni za Fedha Zinazotawala Ukusanyaji wa Mapato Chini ya Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Bodi ya Mapato Zanzibar kwa Faida ya Pande Zote za Muungano

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) wamekubaliana kuwa, kwa vile kodi ya mapato itokanayo na mishahara ya wafanyakazi *(Pay as You Earn - PAYE)* ni suala linalohusu mapato ya Muungano, dai la SMZ kupata fungu kutokana na mapato hayo kwa wafanyakazi wa taasisi za Muungano wanaofanya kazi Zanzibar litekelezwe. Katika kutekeleza makubaliano hayo kuanzia tarehe 1 Julai, 2013 hadi 31 Machi, 2014, jumla ya shilingi **36,750,000,000/=** zimepokelewa na SMZ. Hata hivyo, marekebisho ya kisheria hususan Sheria ya Kodi ya Mapato ya *PAYE* yanahitajika, ili kuweka utaratibu wa wazi zaidi.

Kuratibu Uboreshaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Ajira kwa Taasisi za Muungano ili kuwa na uwiano

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeratibu uboreshaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za ajira kwa Taasisi za Muungano ili kuwa na uwiano katika nafasi za ajira. Sekretarieti za Ajira za SMT na SMZ ziliandaa mapendekezo yaliyopitiwa na Mawaziri wa pande zote za Muungano na kuridhiwa na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano. Mwongozo wa ajira katika Taasisi za Muungano umeandaliwa

na kupitishwa. Mwongozo huo unaendana na Ibara **185** ya Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Desemba, 2013, inayozungumzia uwiano wa ajira kwa washirika wa Muungano.

Kuondoa Vikwazo Katika Utekelezaji wa Masuala ya Muungano

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeratibu utekelezaji wa masuala yanayoendelea kutafutiwa ufumbuzi ambayo ni pamoja na; Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na mgawanyo wa faida ya Benki Kuu, mafuta na gesi asili, usajili wa vyombo vya moto na masuala ya kodi kwa wafanyabiashara.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa suala la mafuta na gesi asili, hoja ilikuwa ni namna ya kugawana mapato yatokanayo na mafuta na gesi asili endapo yatapatikana. Pamoja na hilo, SMZ ilipendekeza kuwa suala la mafuta na gesi asili liondoshwe kwenye orodha ya mambo ya Muungano, na hoja hiyo iliridhiwa na SMT. Mwaka jana nililiarifu Bunge lako tukufu kwamba, Kamati ya Wataalam wa Sekta ya Nishati inayoongozwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa SMT na wa SMZ imeundwa kwa madhumuni ya kufanya uchambuzi wa kisheria (Kitaifa na Kimataifa) juu ya namna biashara hiyo itakavyokuwa na mapato yatakavyogawiwa. Naomba kuliarifu Bunge hili kwamba, Kamati imefanya uchambuzi huo na kuandaa mapendekezo ya utaratibu wa kuiwezesha SMZ kujiandaa kwa biashara hiyo katika misingi ya kisheria na kitaasisi. Ushauri na Mapendekezo ya kazi hiyo yamewasilishwa Serikalini kwa maamuzi.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa usajili wa vyombo vya moto, kazi ya kuoanisha sheria za usajili wa magari zitazowezesha magari yaliyosajiliwa upande mmoja wa Muungano usajili wake utambulike popote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanyika. SMT imezingatia marekebisho hayo kwenye Sheria mpya ya Usalama Barabarani ambayo iko kwenye mchakato wa kupitishwa na Serikali. Aidha, kanzidata *(database)* ya

usajili wa magari unaofanyika SMT na SMZ zitaimarishwa na kuwekwa bayana kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

Uratibu wa Masuala ya Kiuchumi, Kijamii, Kisheria na Mambo Yanayohusiana na Katiba katika Muungano

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu gawio kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Gawio hilo linajumuisha asilimia 4.5 ya Misaada ya Kibajeti (*(General Budget Support – GBS)*, Fedha ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, na Kodi ya Mishahara (PAYE). Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 SMZ imepokea Msaada wa Kibajeti shilingi **27,190,502,190.97/**= kati ya shilingi **32,627,535,000/=** zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2013/14. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014 SMZ imepokea PAYE shilingi **15,750,000,000/=** na fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo shilingi **1,243,925,860/=.** Vilevile, SMT ilichangia shilingi **600,000,000/=** kwenda SMZ kwa ajili ya kufanikisha maadhimisho ya Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki masuala ya kijamii yameratibiwa na kunufaisha wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Serikali zetu kwa ushirikiano zimeendelea kubuni na kutekeleza miradi mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wake. Miradi hiyo inafadhiliwa na Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *Tanzania Social Action Fund - TASAF; Agricultural Sector Development Programme – ASDP, Agricultural Sector Development Program- Livestock ASDP-L* na *Agricultural Sector Support Program- ASSP, Millenium Challenge Account Tanzania – MCAT,* na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya TASAF umeendelea kufanyika katika Wilaya zote za Tanzania Bara na Tanzania

Zanzibar. Kazi zilizofanyika ni pamoja na:- Utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo **22** ambapo kaya maskini **113,297** kutoka katika Vijiji, na Shehia **1,043** zilitambuliwa; Malipo na utimizaji wa masharti ya elimu na afya kwa walengwa wa mpango yamefanyika; Maandalizi ya kukusanya takwimu za awali za Mpango wa *TASAF* Awamu ya Tatu yamefanyika; na Mifumo ya taarifa za uendeshaji yaani (*Management Information System –MIS*) na Masijala ya walengwa imeandaliwa.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14, Programu za kuimarisha huduma za kilimo *ASSP* na Programu ya kuendeleza sekta ya mifugo *ASDP-L* zimetekelezwa katika Shehia **253**; kwa upande wa Unguja ni Shehia **147** na Pemba ni Shehia **106**. Fedha zilizopatikana kwa Programu ya ASSP, ni shilingi **43,138,452. 20,** na kwa Programu ya ASDP-L ni shilingi **222,684,667.53**, kati ya fedha hizo, shilingi **198,494,667.53** ni mchango kutoka *International Fund for Agricultural Development - IFAD* na shilingi **24,190,000/=** ni mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia Programu hizi, wananchi wa Unguja na Pemba wamewezeshwa kupata elimu bora ya kilimo na ufugaji. Aidha, Programu hizi zimesaidia kuongeza uzalishaji wa mazao, kuongeza kipato na uhakika wa chakula.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Program ya *MCA-T* imejumuisha miradi katika sekta tatu **(3)** muhimu za Usafirishaji, Nishati na Maji kwa pande zote mbili za Muungano. Utekelezaji wa miradi hiyo umekuwa wa mafanikio makubwa, kwani karibu miradi yote imekamilika. Wananchi wamefaidika na ujenzi na uboreshaji wa miundombinu na hivyo kusababisha kukua kwa shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo husika. Miradi iliyokamilika kwa upande wa Zanzibar ni: Ujenzi wa njia ya pili ya kupeleka umeme Kisiwa cha Zanzibar (Megawati **100**); Ujenzi wa barabara tano **(5)** za Vijijini Pemba zenye urefu wa jumla ya Kilometa **35** (*Kipangani-Kangagani –Km **2.7**; Chwale- Likoni - Km **1.9**; Mzambarauni- Takao – Pandani – Finya – Km **7.9**;*

*Mzambarauni Karimu – Finya- Mapofu – Km **8.7**; na Bahanasa – Daya – Mtambwe – Km **13.8***).

Kuelimisha Umma Kuhusu Muungano

23. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na jamii yenye uelewa wa masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano, Ofisi iliandaa Makongamano manane **(8)** ya kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano. Makangamano hayo yalifanyika kuanzia mwezi Septemba 2013 hadi mwezi Februari, 2014 katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Dodoma, Zanzibar, Mbeya na Iringa. Makongamano hayo yalihusisha wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu, baadhi ya viongozi wa Serikali za SMT na SMZ na Wananchi kwa ujumla. Makongamano hayo yalitoa fursa za kubadilishana mawazo juu ya umuhimu wa kutatua changamoto zinazo ukabili muungano wetu ili tuweze kuulinda na kuuimarisha.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliandaa na kuchapisha nakala **2,000** za Jarida la Muungano Wetu; nakala **7,000** za vipeperushi; nakala **5,000** za Jarida Maalum la Miaka **50** ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; na nakala **5,000** za Kitabu cha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar - Historia katika Picha na kuzisambaza kwa wadau. Lengo la kuandaa machapisho hayo ni kukuza uelewa wa jamii katika masuala ya Muungano. Machapisho hayo yanaelezea historia, mafanikio, changamoto za Muungano, jitihada zilizochukuliwa kutatua changamoto hizo, na matarajio ya baadae. Pamoja na juhudi hizo, ilibainika kwamba elimu zaidi inahitajika pamoja na uwepo wa uwazi wa mambo ya Muungano, ili kujenga upeo wa uelewa kwa jamii ya Watanzania.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha Maadhimisho ya Miaka **50** ya Muungano, Ofisi imeratibu Makongamano mawili **(2)** yaliyofanyika Zanzibar. Moja ni kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki na jengine kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Makongamano haya yalihusisha Wadau kutoka katika makundi ya wasomi, wanasiasa, makundi

maalum na taasisi za SMT na SMZ. Pamoja na Makongamano hayo, Taarifa ya Miaka **50** ya Muungano iliandaliwa na Kamati iliyoundwa na wajumbe kutoka Wizara na Taasisi za Muungano kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Vile vile, Ofisi iliratibu Maonesho ya Miaka 50 ya Muungano yaliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Ushirikiano Katika Masuala Yasiyo ya Muungano

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali zote mbili **(2)** zilishirikiana kikamilifu kufanikisha maadhimisho na kusherehekea miaka **50** ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Taasisi nyingine za Muungano zilishiriki katika maonesho ya maadhimisho hayo, kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu mafanikio na changamoto zilizopo.

Miaka 50 ya Muungano

27. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, mwaka huu, tumeshuhudia Muungano wetu ukitimiza miaka **50** tangu kuasisiwa kwake. Ni ukweli ulio wazi kuwa, Muungano upo kwa sababu ya uamuzi makini na wa busara uliofanywa na viongozi waasisi wa Taifa letu, **Mwalimu Julius Kamabarage Nyerere** aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Tanganyika na **Mzee Abeid Amani Karume** aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Tunaposherehekea na kuadhimisha miaka **50** ya Muungano, hatuna budi kutambua, kupongeza na kuthamini uongozi wao, hasa kwa kuona mbali kuhusu umuhimu wake, na mchango mkubwa walioutoa katika kuasisi na kujenga Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na juhudi za waasisi hao, hatuna budi kuwashukuru Viongozi wa Kitaifa katika Awamu zote za

Uongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuenzi Muungano wetu.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** kipindi cha miaka **50** ya Muungano wetu kimekuwa na mafanikio mengi katika nyanja za kiuchumi, ulinzi na usalama, kisiasa na kijamii kama yalivyoainishwa kwenye Kitabu cha Taarifa ya Miaka Hamsini ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Malengo ya Mwaka 2014/2015

29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Ofisi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya uratibu wa masuala ya Muungano na kudumisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika kutekeleza hayo, shughuli za Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano pamoja na vikao vinavyohusika vitaratibiwa ili kurahisisha utekelezaji wa masuala hayo.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea kufanya ufuatiliaji wa miradi ya kijamii iliyopo na mipya ambayo ni; *ASSP, ASDPL, TASAF* na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, ili kubaini manufaa na mapungufu yanayopatikana kwa kuwepo kwa miradi hiyo. Vile vile, ushirikiano baina ya Wizara na Taasisi zisizo za Muungano zenye kazi zinazoshabihiana kati ya SMT na SMZ utaimarishwa.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** suala la elimu kwa umma litapewa msukumo kwa kushirikiana na Kamati za ushauri za Mikoa na Wilaya, ili watanzania wapate uelewa mkubwa zaidi wa historia ya Muungano, na hali ilivyo kwa wakati huu.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa nchi yetu ipo katika mchakato wa kuandika Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi

itatekeleza masuala yote yanayohusu Muungano yatakayotokana na Katiba hiyo.

III. HIFADHI YA MAZINGIRA

MAELEKEZO YA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 – 2015 NA UTEKELEZAJI WAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2013/14

33. ***Mheshimiwa Spika,*** ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015 Ibara ya **194** inaelekeza Serikali kutekeleza masuala ya Hifadhi na kusimamia mazingira hapa nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14 utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

"Kuimarisha zoezi la kitaifa la kupanda miti pamoja na miti ya asili kila mwaka katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Viongozi wa vitongoji, mitaa, vijiji na kata watakiwe kuikagua mara kwa mara miti iliyopandwa ili kuhakikisha inakua. Aidha, miti ipandwe katika maeneo ya shule, barabara, zahanati za vijiji, vituo vya afya na makazi ya watu. Wakuu wa maeneo hayo wahakikishe lengo la kupanda miti linafanikiwa".

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji kwa kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti milioni **1.5** kwa mwaka kwa kila Halmashauri ya Wilaya. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, Ofisi imepokea taarifa za Mikoa **20** kuhusu miti iliyopandwa na kumea mwaka wa fedha 2012/13. Taarifa hizo zinaonesha kuwa miti **209,252,221** ilipandwa na kati ya hiyo miti **142,868,916** imestawi, sawa na asilimia **68.28** ya miti iliyopandwa (***Kiambatisho Na.1*** *ni Taarifa za upandaji miti kitaifa kwa mwaka wa fedha 2012/13).* Halmashauri zilizopanda miti na kustawi kwa zaidi ya asilimia **80** ni **37** ambazo ni Wilaya za Mbinga, Ileje, Kyela, Jiji la Mbeya, Mbeya Vijijini, Mbozi, Momba, Mufindi, Liwale, Kilwa, Sumbawanga, Mpanda, Mlele, Tarime, Jiji la Mwanza, Ilemela, Magu, Ludewa, Njombe, Halmashauri ya Mji wa Njombe, Uyui, Ulanga, Kilombero, Manispaa ya Morogoro, Mvomero, Morogoro Vijijini, Biharamulo, Misenyi, Bukoba Vijijini, Muleba, Manispaa ya Bukoba, Ngara, Kilindi, Pangani,

Mkinga, Handeni na Korogwe. Mikoa ambayo Halmashauri zake hazijawasilisha taarifa za upandaji miti kwa mwaka wa fedha 2012/13 ni Arusha; Dar es Salaam; Simiyu; Singida; na Geita. Naipongeza Mikoa ambayo wilaya zake zimevuka lengo la upandaji miti, na nahimiza mikoa mingine kuongeza juhudi ili kulinda mazingira ya nchi yetu.

35. ***Mheshimiwa Spika***, mashindano ya Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti yameendelea kuhamasishwa nchini katika ngazi za Kaya; Vijiji; Kata; Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa; Mikoa; Shule za Msingi na Sekondari; Vyuo vya Mafunzo/Utafiti; Taasisi za Kijeshi; Taasisi/Vikundi vya Uhamasishaji na Uwezeshaji; na Taasisi/Kampuni za Uhamasishaji na Uwekezaji. Tuzo hii inayotolewa kila baada ya miaka miwili (2), kwa mwaka huu, itatolewa tarehe 5 Juni, katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, ambapo kitaifa yatafanyika Mwanza. Mikoa iliyoshiriki katika mashindano haya kwa mwaka huu ni Dodoma, Iringa, Kagera, Katavi, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mbeya, Mwanza, Mara, Mtwara, Morogoro, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu na Tanga. Napenda kuipongeza mikoa hii kwa kushiriki katika mchakato wa Tuzo hii.

“Serikali za vijiji na Halmashauri za Wilaya na Manispaa zitunge sheria ndogo za hifadhi ya misitu”

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, Halmashauri za Wilaya zilizotunga Sheria ndogo za hifadhi ya misitu na mazingira ni Halmashauri za Wilaya za Moshi, Mpanda, Kalambo, Uvinza, Kasulu na Kibondo zimeanza kutumia Sheria ndogo katika kuainisha vyanzo vya maji na kuvitunza. Aidha, Halmashauri za Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma zinaendelea kuandaa sheria ndogo za hifadhi ya mazingira. Vilevile, Halmashauri nyingine zinaendelea kufuatiliwa na kusisitizwa kuhusu umuhimu wa kutumia sheria ndogo za kulinda na kuhifadhi mazingira.

“Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Mazingira katika vyanzo vya maji na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa usafi katika fukwe”

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira imeendelea kutekeleza Mkakati wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani kama ilivyoainishwa katika Aya **78** ya Hotuba ya kitabu cha Bajeti.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio katika kutekeleza Mkakati huu ni kuimarika kwa mazingira ya bahari na fukwe, kuongezeka vipato vya wananchi kupitia miradi iliyotekelezwa, kutolewa kwa elimu kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira, na kupungua kwa uchafuzi wa mazingira. Aidha,mafanikio mengine ni kupatikana kwa taarifa za mifumo ya ikolojia ya ukanda wa Bahari ya Hindi ambazo zimetumika kuandaa taarifa ya hali ya mazingira ya Pwani, na ramani zinazoonesha maeneo muhimu yanayohitaji kuhifadhiwa. Vilevile, taarifa hizo zitasaidia katika kuandaa mpango wa usimamizi wa mazingira ya bahari.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** mambo mengine yaliyotekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14 ni Ukaguzi na tathmini ya ujenzi kandokando ya Ziwa Viktoria uliofanyika katika maeneo ya Mkuyuni, Capri-point na Igombe – Mwanza, na waliojenga kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira walipewa Hati ya Katazo ili wasiendelee kujenga ndani ya mita **60** kutoka fukwe za Ziwa hilo. Ukaguzi wa awali wa Mto Mkundi uliopo Morogoro na eneo la dakio (*catchment area*) ulifanywa na kubaini uharibifu uliosababishwa na mafuriko; Taarifa za hali ya Milima katika mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara iliandaliwa; na Tathmini ya hali ya chemichemi za maji katika eneo la Themi - Arusha ilifanyika.

40. ***"Serikali ichukue hatua ya kuandaa sera na kutunga sheria itakayosimamia matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa Mazingira"***

41. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kupitia Programu ya Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira iliiwezesha Wizara ya Nishati na Madini kuandaa Mpango wa Mazingira wa Sekta ya Nishati na Madini. Mpango huu utaiwezesha Wizara kuandaa Sera ya Nishati Mbadala. Aidha, Wizara ya Nishati na Madini inaandaa Sera ya Uendelezaji wa Nishati itokanayo na Biofueli (*Biofuels Development Policy*). Sera hizi zitawezesha kupungua kwa matumizi makubwa ya kuni na mkaa ambayo huongeza kasi ya uharibifu wa mazingira. Sanjari na zoezi hilo, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara hiyo inaandaa Tathmini ya Mazingira Kimkakati kuhusu Sera ya Uendelezaji wa Biofueli.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2014/15 Ofisi itaendelea na mchakato wa kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997. Katika mapitio hayo, pamoja na mambo mengine suala la nishati mbadala litazingatiwa kama hatua ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ili kuhifadhi mazingira.

"Serikali kupunguza gharama za vifaa vya nishati mbadala ili wananchi wanaojenga nyumba za kisasa vijijini watumie nishati hiyo badala ya kuni na mkaa wa miti"

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusimamia uamuzi wake wa kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani katika vifaa vya gesi na umeme ili wananchi waweze kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na hivyo kunusuru mazingira yetu. Katika kutekeleza hilo, Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa vifaa vya nishati mbadala kama vile, upepo na jua ilipunguzwa kwa asilimia 1**8**. Aidha, mwaka 2013 Serikali ilipunguza gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya vijijini kutoka takriban shilingi **500,000** hadi shilingi **27,000** tu, kwa lengo la kupunguza matumizi

ya kuni na mkaa. Aidha, Washirika wa Maendeleo yakiwemo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakichangia jitihada za Serikali kwa kuwezesha upatikanaji wa nishati mbadala vijijini.

"Serikali iimarishe usimamizi wa viwanda na biashara ili kutochafua mazingira"

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2013/14, Ofisi kupitia Baraza ilifanya ukaguzi wa viwanda, migodi na biashara **105** katika mikoa ya Mwanza, Morogoro, na Dar es Salaam. Hatua za kisheria zilichukuliwa kwa viwanda na shughuli zilizobainika kukiuka Sheria ya Usimamizi wa Mazingira sura 191, ikiwa ni pamoja na kutoa notisi za kufanya marekebisho; kulipa faini; kufungiwa na kupewa masharti ya kutekeleza, ili kuboresha hali ya mazingira. (Ufafanuzi wa kina upo katika Aya ya **95** hadi **102** ya Hotuba ya kitabu cha Bajeti.).

Kutekeleza Mradi wa Vijiji vya Mfano vya Hifadhi ya Mazingira (Eco-Villages)

45. ***Mheshimiwa Spika,*** awamu ya pili ya Mradi wa Vijiji vya Mfano (*Eco-villages*) unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya, umeanza kutekelezwa kwa gharama ya takriban *Euro* milioni **8**, sawa na shilingi bilioni **16**. Mradi huu unatekelezwa katika Kanda za Maeneo ya Pwani na Ukanda wa Chini, Maeneo ya Miinuko yenye mvua nyingi kiasi; na Maeneo ya Kanda Kame. Mchakato wa kupata Taasisi za kutekeleza Mradi huu umeanza ambapo Taasisi **71** ziliandaa na kuwasilisha Andiko la Wazo la Mradi (*Concept Notes*). Taasisi **16** zilifanikiwa kuandaa maandiko yaliyokidhi vigezo na tayari zimetaarifiwa kuandaa Andiko Kamili la Mradi (*Project Proposals)*, ambapo miradi sita (**6**) itakayokidhi vigezo inatarajiwa kupitishwa. Aidha, kila mradi unakadiriwa kuwa na gharama ya takriban *Euro* milioni **1** hadi milioni **1.5** kutegemea ukubwa wa kila mradi.

"Kufanya Tathmini ya Athari za Kimazingira Katika Miradi ya Ujenzi"

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, limeendelea kusimamia na kuhakikisha kwamba miradi ya ujenzi inafanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira. Kwa mwaka wa fedha 2013/14, jumla ya miradi **935** ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa TAM. Kati ya Miradi hiyo, **396** ni ya ujenzi na Miradi **298** ilipatiwa Hati (*Environmental Impact Assesment-IA Certificates).* Miradi iliyobaki imerejeshwa kwa wahusika kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho.

UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/14 NA MALENGO YA MWAKA 2014/15

47. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015, Ofisi katika kipindi hicho ilitekeleza yafuatayo:-

Elimu ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

48. ***Mheshimiwa Spika***, Maadhimisho yanayohusu masuala ya mazingira hutumiwa kama ni fursa ya kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira. Maadhimisho hayo ya kitaifa ni; Siku ya Ozoni Duniani; Siku ya Mazingira Duniani; Siku ya Mazingira ya Afrika; Siku ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame; na Wiki ya Utumishi wa Umma. Katika maadhimisho haya kila mwaka, elimu ya mazingira hutolewa kwa kutumia hotuba za viongozi, vipeperushi, mabango, machapisho na vitabu vyenye ujumbe kuhusu masuala ya mazingira. Aidha, Ofisi imeendelea kutoa elimu ya mazingira kupitia warsha, semina na makongamano mbalimbali yanayofanyika nchini. Elimu ya mazingira hutolewa pia kupitia vipindi vya redio, luninga, makala kwenye magazeti, na kupitia tovuti ya Ofisi.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya nakala **3,000** za Mpango Kazi wa Taifa wa Mazingira (*National Environmental Action Plan - NEAP)* zilichapishwa na kusambazwa kwa Wizara zote na Mikoa yote nchini. Aidha, Ofisi imechapisha na kusambaza nakala **3,600** za Mwongozo wa Kuhuisha Mabadiliko ya Tabianchi Katika Sera na Mipango ya Kisekta; nakala **3,600** za mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya mabadiliko ya tabianchi; na nakala **3,600** za Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano ya Mabadiliko ya Tabianchi.

Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliidhinisha Tathmini ya Mazingira Kimkakati kuhusu Mpango Kabambe wa Taifa wa Sekta ya Uchukuzi na Biashara nchini. Aidha, Ofisi inaendelea kuratibu tathmini nyingine za mazingira kimkakati kuhusu sera na miradi kama ifuatavyo:- Sera ya Uendelezaji wa Biofueli; Mradi wa Kujaza eneo la Pwani ya Dar es Salaam; Mradi wa kuendeleza Mji wa Kisasa katika eneo la Tengeru - Halmashauri ya Wilaya ya Meru; na Mradi wa Uendelezaji wa Mji wa Kisasa katika eneo la Kibada, Kigamboni. Katika kuongeza ufanisi wa uandaaji wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati, Ofisi inaandaa Mwongozo wa uandaaji wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati utakaokamilika mwezi Juni, 2014.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imetoa ushauri wa kitaalam kwa Wizara ya Maji; na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika kuandaa mikakati na mipango ya kisekta ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Halmashauri za Wilaya **16** katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Tanga na Mtwara zimejengewa uwezo wa kutathmini athari za mazingira na zimewezeshwa kuandaa mipango kazi ya usimamizi wa mazingira.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kutekeleza Programu ya Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira-*Environmental Management Act-Institutional Support Programme (EMA-ISP)*, na kuandaa Kanuni za Mbinu za Kiuchumi za Usimamizi wa Mazingira; Kanuni za Kusimamia Kemikali Hatari za Vimiminika kutoka Viwandani; Kanuni za Kusimamia Taka Zitokanazo na Vifaa vya Umeme na Kielektroniki; Kanuni za Uandaaji wa Mipango Kazi ya Mazingira ya Sekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Kanuni za Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi pia imeandaa Miongozo sita **(6)** chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura **191** nayo ni:- Mwongozo wa Upangaji Mipango ya Mazingira na Ardhi; Mwongozo wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi Oevu; Mwongozo wa Usimamizi na Matumizi Endelevu ya Nyanda za Malisho ya Mifugo; Mwongozo wa Jinsi ya Kukabiliana na Maafa ya Kimazingira; Mwongozo wa Kujumuisha Masuala ya Jinsia katika Mazingira;

na Mwongozo wa Wakaguzi wa Mazingira. Katika jitihada za kuanzisha Mfuko wa Mazingira, Rasimu ya Mwongozo wa Kusimamia Fedha za Mfuko (*Financial Procedure Guidelines*); na Rasimu ya Mwongozo kwa ajili ya kusimamia uendeshaji wa Mfuko (*Operational Manual*) zimeandaliwa. Uteuzi wa majina ya Wajumbe wa Bodi ya Mfuko unaendelea.

55 Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2014/15, tathmini ya vyanzo vya fedha vya Mfuko itafanyika na mapendekezo yatawasilishwa Serikalini kwa maamuzi. Aidha, washirika wa maendeleo watahamasishwa kuchangia katika Mfuko huu.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inaelekeza uundwaji wa Baraza la Rufaa la Mazingira. Tayari Msajili na wajumbe wa Baraza wameteuliwa. Aidha, uteuzi wa Mwenyekiti wa Baraza unasubiri maamuzi ya mamlaka husika. Katika kipindi hiki, vigezo na taratibu (*Rules of procedures*) za uendeshaji wa Baraza zimeandaliwa na Baraza litaanza kazi rasmi baada ya taratibu zote kukamilika.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mchakato wa kuandaa Ripoti ya Pili ya Hali ya Mazingira nchini umekamilika na Ripoti ipo katika hatua za kuchapishwa. Ripoti hii inatoa mwelekeo wa hali ya mazingira hapa nchini, hatua zilizochukuliwa kukabiliana na uharibifu wa mazingira na kuweka mipango itakayoshughulikia changamoto za uharibifu wa mazingira.

Utekelezaji wa Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika

56. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2013/14 Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu endelevu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika inayohusisha nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Tanzania na Zambia. Miradi mitatu **(3)** inayotekelezwa chini ya Programu hii ni:- Mradi wa Usimamizi wa Bonde la

Ziwa Tanganyika (*Catchment Management*); Mradi wa Usimamizi wa Majitaka katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji; na Mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji sita **(6)** vya mfano ambavyo, ni Nyange (Kibondo), Titye (Kasulu), Ilagala (Kigoma), Karema (Mpanda), Korongwe (Nkasi) na Kisumba (Sumbawanga).

57. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka **6** (kuanzia Septemba, 2008 hadi Desemba, 2013) cha utekelezaji wa programu hii, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:- Kukamilika kwa ujenzi wa barabara zenye urefu wa Km **63.1** kwa kiwango cha changarawe katika Wilaya za Nkasi, Mpanda, Sumbawanga, Uvinza na Kigoma. Barabara hizi ni pamoja na zile zilizojengwa katika vijiji vya jamii za wavuvi vilivyopo kandokando ya Ziwa Tanganyika, ambavyo havikuwa na miundombinu ya barabara kabisa, vilitegemea usafiri wa majini kama njia pekee ya kufikisha mazao yao sokoni.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli nyingine zilizokamilishwa ni: - Ujenzi wa kiwanda kidogo cha kuchakata mafuta ya mawese; Uchimbaji wa kisima kirefu cha maji katika kijiji cha Ilagala - Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza; na Ujenzi wa soko la kisasa la samaki Kibirizi. Mradi pia umekamilisha ujenzi wa zahanati na nyumba ya mganga katika kijiji cha Isengule; Ujenzi wa vyumba vinne **(4)** vya madarasa, ambapo viwili **(2)** vimejengwa kijiji cha Isengule na viwili **(2)** kijiji cha Itetemya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda. Ujenzi wa wodi ya wazazi katika Kijiji cha Samazi Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo umekamilika. Miche **8,500** ya miembe inayokomaa kwa muda mfupi imeoteshwa katika Halmashauri za Mpanda **(5,000),** Kasulu **(500),** Nkasi **(1,000),** Kibondo **(1,000)** na Kalambo **(1,000)** kwa lengo la kupunguza uharibifu wa mazingira, na umaskini kwa kuanzisha shughuli mbadala za kiuchumi. Aidha, Mradi umegawa mizinga **70** ya nyuki ya kisasa kwa vikundi katika vijiji sita **(6)** vya mfano. Shughuli zinazoendelea kukamilishwa ni Ujenzi wa mialo minne **(4)** katika Halmashauri za Nkasi (Kirando); Mpanda (Ikola); Kigoma/Ujiji (Kibirizi); na

Uvinza (Muyobozi); na Ukarabati wa mtambo wa kuzalisha barafu *(Ice plant)* katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

59. ***Mheshimiwa*** **Spika,** pamoja na hayo utafiti wa kubaini maeneo yanakopatikana kwa wingi samaki wa mapambo na aina nyingine za samaki ndani ya Ziwa Tanganyika ulifanywa na TAFIRI. Kupitia utafiti huo, aina mbili za samaki wa mapambo ambao wako katika hatari ya kutoweka walionekana. Utafiti huu ulipendekeza maeneo wanakopatikana samaki hao yahifadhiwe. Hivyo, Mpango wa Usimamizi wa Hifadhi ya maeneo hayo yaliyobainishwa umeandaliwa.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** ufadhili wa Programu ulifikia ukomo tarehe 31 Desemba, 2013, Mpango Mkakati unaoainisha namna shughuli za Mradi zitakavyoendelezwa kwa kuhuishwa katika mipango na bajeti za Wilaya husika uliandaliwa, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya zilizokuwa zinatekeleza miradi chini ya programu hii

61. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2014/15 Ofisi itaendelea kufuatilia maendeleo ya vikundi vya kijamii katika vijiji sita vya mfano vilivyopewa fedha na mradi; Kuendelea kufuatililia utekelezaji wa Sheria ndogo za usimamizi wa mazingira na Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika vijiji vya mfano; Kuendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa hifadhi ya mazingira; na Kuendelea kushirikiana na nchi za Burundi, Democratic Republic of Congo, na Zambia chini ya Mamlaka ya Ziwa Tanganyika katika kubuni na kuandaa programu nyingine ya awamu ya pili itakayotekelezwa na nchi wanachama.

Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai

62. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ilifanya uratibu wa maandalizi ya Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Hifadhi ya Bioanuai kwa kuzingatia Mpango Mkakati Mpya wa Kimataifa wa mwaka 2011 hadi 2020; uratibu wa majadiliano ya wadau kuhusu kuridhia Itifaki ya Nagoya inayohusu

kusimamia Upatikanaji na Mgawanyo Sahihi wa Faida Zitokanazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki; na Itifaki ya Nagoya Kuala-Lumpur kuhusu Uwajibikaji Kisheria Dhidi ya Athari zitokanazo na Matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa.

Pamoja na hayo, Ofisi imekamilisha uandaaji wa Ripoti ya Tano ya kitaifa kuhusu utekelezaji wa Mkataba. Ripoti hii imebainisha hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na uharibifu wa Bioanuai katika maeneo ya nchi kavu na majini.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Bioanuai pamoja na Itifaki zake na kukamilisha mchakato wa kuridhia Itifaki ya Nagoya inayohusu Kusimamia Upatikanaji na Mgawanyo Sahihi wa Faida zitokanazo na Rasilimali za Kijenetiki; na Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala- Lumpur kuhusu Uwajibikaji Kisheria Dhidi ya Athari Zitikanazo na Matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa.

64. **Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Itifaki ya Cartagena Kuhusu Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa umeendana na shughuli za kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili Mfumo wa Usimamizi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa (*National Biosafety Framework, 2007*) kwa lengo la kuwawezesha wananchi wengi kuelewa maudhui ya mfumo huo, namna unavyofanya kazi na nafasi yao katika utekelezaji wake. Aidha, Maabara za taasisi tano (**5**) zinazohusika na udhibiti na utafiti zimejengewa uwezo kwa kuzipatia vitendea kazi *(Genetically Modified Organisms - laboratory equipment)* vitakavyosaidia shughuli za utambuzi na ung'amuzi wa mazao au viumbe ambavyo vimefanyiwa mabadiliko kwa kutumia njia ya uhandisi - jeni.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi zilizofaidika na msaada huo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mamlaka ya Chakula na Dawa, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar

na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Mikocheni. Aidha, Mradi umejenga uwezo wa Ofisi na Wizara za kisekta ili shughuli hizi ziwe endelevu baada ya muda wa mradi huu kukamilika.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15, Ofisi itaendelea na kukuza uelewa kwa wananchi juu ya matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa. Aidha, Ofisi itaandaa na kusambaza miongozo ya usafirishaji wa bidhaa na kilimo cha mazao yatokanayo na biotejinolojia ya kisasa.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Kuhusu Utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na Itifaki ya Kyoto Serikali imeendelea kutekeleza Mradi wa Kuhuisha masuala ya mazingira na kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika sera na mipango ya maendeleo ya Serikali. Vile vile, tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta za kilimo, mifugo na misitu imefanyika na mradi wa majaribio wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika sekta hizi tatu kuandaliwa. Mradi huu utatekelezwa katika Wilaya ya Singida Vijijini kwenye Vijiji vya Mgori, Mughunga na Unyampanda.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa Programu ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Afrika (*Africa Adaptation Programme - AAP*). Kazi zifuatazo zilitekelezwa:- Mafunzo yalifanyika kwa Maafisa Mipango **(18)** kutoka Wizara, Idara, na Taasisi za Serikali kuhusu namna ya kuhuisha masuala ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika sera, mipango na mikakati; Mwongozo kwa ajili ya kuhuisha masuala ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwenye Sera, Mipango na Programu za kitaifa za kisekta; Mwongozo wa Kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa jamii ya wakulima na wafugaji; Mkakati wa Kitaifa wa Mawasiliano kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi; Miradi minne **(4)** ya maji ya majaribio kwa ajili ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika Wilaya za Mbinga, Igunga, Misenyi, na Nungwi - Zanzibar ilikamilishwa.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Maeneo ya Pwani ya Dar es Salaam wenye thamani ya takriban Dola za Marekani **5,000,000/=** umeanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2013/14. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kufanya tathmini ya athari kwa mazingira; kuandaa taarifa ya awali ya Mradi (*baseline study*) na kuanzisha kamati elekezi ya usimamizi wa Mradi.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi za Mradi zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni pamoja na kuanza ukarabati na uimarishaji wa ukuta wa Bahari (urefu wa Kilomita **1.35**) ulioharibika katika maeneo ya Ocean Road na Kigamboni (Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere); kuanza ukarabati wa miundombinu ya majitaka ya katikati ya Jiji la Dar es Salaam; kusambaza teknolojia za nishati mbadala na majiko banifu kwa kaya **3,000** katika Manispaa za Ilala na Temeke; kukuza uelewa wa jamii kuhusu nishati jadidifu na banifu; kuandaa Mkakati wa kupunguza uharibifu wa mikoko Jijini Dar es Salaam; kuboresha na kukarabati matumbawe yaliyoharibika katika maeneo ya Dar es Salaam; kukuza uelewa wa wavuvi na maafisa ugani wa uvuvi kuhusu njia endelevu za uvuvi na kutunza matumbawe; na kutengeneza Mpango Kazi wa Utunzaji wa Pwani ya Dar es Salaam (*Ecosystem Based Integrated Coastal Area Management Action Plan*).

71. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi inatekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii za Pwani ya Bahari ya Hindi Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kutokana na Kuongezeka kwa Kina cha Bahari. Mradi huu unathamani ya jumla ya Dola za Marekani milioni **3.3**, na unahusisha Wilaya za Bagamoyo, Pangani, Rufiji na Zanzibar. Maafisa **20** kwa kila Halmashauri za Wilaya za Bagamoyo na Rufiji walipatiwa mafunzo kuhusu kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, kazi zifuatazo zitatekelezwa:- Kukarabati ukuta kwa lengo la kuzuia maji ya

bahari kuingia katika miji ya Pangani; Kuchimba visima vya maji baridi katika eneo la pwani ya Bagamoyo ikiwa ni hatua ya kukabiliana na tatizo la visima vya maji vilivyokuwepo kuingiliwa na maji ya chumvi ya bahari; Kupanda mikoko katika eneo la Delta ya Msimbati Wilaya ya Rufiji kwa lengo la kuzuia mmomonyoko wa fukwe za bahari unaotokana na kuongezeka kwa kina cha bahari na kuingia kwa maji ya bahari katika mashamba ya wananchi; na Kuendelea kujenga uwezo na uelewa wa watendaji na jamii za Halmashauri za Wilaya husika.

Utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi Mpya wa Mkataba kwa kipindi cha mwaka 2013 hadi 2017. Katika kutekeleza Mpango huo, Ofisi kwa kushirikiana na nchi wanachama na *UNEP* imeanza mchakato wa kuandaa Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Kikanda ya Ukanda wa Pwani na Bahari. Vilevile, Ofisi imeendelea kukamilisha taratibu za kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Nairobi na Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi, kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu. Aidha, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa Mito na Mabwawa kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya na Maafisa Mabonde. Shughuli hizi zitaendela kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2014/15.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(Global Environment Facility – GEF)* chini ya usimamizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP), ulifadhili miradi midogo **35** yenye thamani ya shilingi

3,649,624,929. Miradi iliyopata ufadhili huo iko katika Mikoa ya Morogoro, Ruvuma, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Mara, Pwani, Kagera, Rukwa, Iringa, Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma, Manyara, Tabora na Zanzibar. ***"Kiambatisho Na. 2*** ni orodha ya Miradi midogo iliyopata ufadhili"

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi itaongeza jitihada zaidi katika kuhimiza na kushauri Asasi za Kiraia kuandaa miradi mingi zaidi ili kunufaika na fedha kutoka Mfuko wa Dunia wa Mazingira. Ofisi pia itaendelea kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi inayoendelea kutekelezwa chini ya ufadhili wa GEF.

Uratibu wa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeratibu maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo hufanyika tarehe 5 Juni ya kila mwaka. Mwaka 2014 maadhimisho haya yatafanyika kitaifa mkoani Mwanza. Aidha, kaulimbiu ya Maadhimisho ya mwaka huu Kimataifa ni: "**Raise Your Voice not the Sea Level"** ikiwa na maana kwamba ***Ongeza Sauti yako Kutetea Mazingira na Sio Kuongeza Kina cha Bahari.*** Ujumbe huu unahimiza umuhimu wa kuhifadhi na kulinda rasilimali za mazingira zinazosababisha kuongezeka kwa kina cha bahari.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mkataba wa Montreal Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni Angani umehusisha kuwajengea uwezo mafundi mchundo jinsi ya kutumia njia bora ya kuhudumia majokofu na viyoyozi katika viwanda vya samaki vilivyoko Kanda ya Ziwa, na Kuratibu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Ozoni tarehe 16 Septemba, 2013 yaliyofanyika Jijini Mwanza.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kuendesha Warsha ya Mafunzo kwa mafundi mchundo **50** na Wakufunzi **70** wa Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) kuhusu teknolojia mbadala na rafiki kwa tabaka la Ozoni na katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha,

Mpango wa kitaifa wa kupunguza/kusitisha matumizi ya kemikali aina ya *Hydrochlorofluorocarbons* (HCFCs) nchini kwa kufuata ratiba iliyowekwa na Mkataba umeendelea kutekelezwa; takwimu za uingizaji nchini na matumizi ya kemikali hizi na teknolojia mbadala katika majokofu na viyoyozi zimekusanywa; na Taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mkataba imeandaliwa na kuwasilishwa katika Sekretarieti ya Mkataba.

77. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi itaratibu utekelezaji wa Mkataba huu nchini kwa kuendelea kukuza uelewa wa jamii kuhusu utekelezaji wa Mkataba na udhibiti wa kemikali zinazoharibu tabaka la Ozoni (ODS); Kuendesha mafunzo ya wadau juu ya utekelezaji wa sheria na kanuni za kudhibiti matumizi ya kemikali zisizo rafiki kwa tabaka la Ozoni; Kutekeleza Mpango wa kitaifa wa kupunguza/kusitisha matumizi ya kemikali aina ya Hydrochlorofluorocarbons - HCFCs nchini kwa kufuata ratiba iliyowekwa na Mkataba; Kukusanya takwimu za uingizaji na matumizi ya kemikali zisizo rafiki kwa tabaka la Ozoni nchini; na Kuwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mkataba nchini katika Sekretarieti ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Stockholm wa Kudhibiti Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa muda mrefu - *Persistent Organic Pollutants* (POPs) ulitekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa vikundi kazi vya wataalamu watakao husika na ukusanyaji wa taarifa za uingizaji, matumizi na uchakavu wa kemikali za awali na kemikali mpya zilizoongezwa kwenye Mkataba ambapo jumla ya wataalamu **16** walishiriki. Aidha, uchambuzi wa kuainisha Kikosi Kazi na majukumu katika kufanya mapitiao ya Mpango Kazi wa Kitaifa wa Mkataba yamefanyika.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi itaendelea kuratibu mapitio ya Mpango wa Taifa wa Usimamizi wa Mkataba wa Stockholm ikiwa ni pamoja na kukamilisha ripoti ya ukusanyaji takwimu za kemikali zinazozibitiwa na Mkataba huu; Kufanya ukaguzi wa maeneo yaliyoharibiwa na kemikali za sumu zinazodumu kwa muda mrefu katika

mazingira; Kukuza uelewa kuhusiana na usimamizi bora wa kemikali hizi; na Kufanya mapitio ya Mpango wa utekelezaji wa Mkataba na kuuwasilisha kwenye Sekretarieti ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka za Sumu Baina ya Nchi na Nchi (Mkataba wa Basel) na Mkataba Unaozuia Uingizaji wa Taka za Sumu Barani Afrika (Mkataba wa Bamako) ulifanyiwa kazi kwa kufanya utafiti wa changamoto zilizopo katika usimamizi endelevu wa mafuta machafu hususan katika gereji za kutengeneza magari na vituo vya kupokelea mafuta machafu katika Jiji la Dar es Salaam. Filamu kuhusu shughuli za usimamizi wa taka sumu katika Jiji la Dar es Salaam hususan mafuta machafu, betri chakavu na vifaa vya umeme na elektroniki, na madawa ya kilimo na viuatilifu inatayarishwa. Aidha, warsha ya wadau ya kubadilishana uzoefu katika matumizi ya nyenzo na mbinu za kiuchumi katika usimamizi endelevu wa mafuta machafu iliyoshirikisha Manispaa ya Jiji la Dar es Salaam na kampuni wanaorejeleza mafuta machafu ilifanyika.

Mheshimiwa Spika, Katika juhudi za Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame miradi mitatu **(3)** inayolenga kupunguza uharibifu wa ardhi na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame (*Sustainable Land Management on Reducing Deforestation Land Degradation and Drought*) inatekelezwa chini ya ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*Global Environment Facility – GEF*) kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (*United Nation Development Programme - UNDP*).

79. Mradi wa kwanza ni wa Kuimarisha Usimamizi Endelevu wa Ardhi Nchini unaohusisha kukamilisha Taarifa ya Hali ya Uharibifu wa Mazingira nchini Kuhuisha Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na kuenea kwa hali ya Jangwa na Ukame ili uendane na Mkakati wa Miaka **10** (*2008 - 2018*) wa utekelezaji wa Mkataba; Kukamilisha Mpango Mkakati wa kuhuisha Masuala ya kifedha katika masuala ya Usimamizi Endelevu wa Ardhi; na kukamilisha maandalizi ya Ripoti ya Tano ya utekelezaji wa Mkataba ambayo itawasilishwa Sekretarieti ya Mkataba mwezi Juni, 2014.

Ripoti hizi huandaliwa kila baada ya miaka miwili (**2**) kwa mujibu wa Mkataba.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa pili ni wa Kupunguza Uharibifu wa Ardhi katika Miinuko ya Mkoa wa Kilimanjaro (*Reducing Land Degradation on the Highlands of Kilimanjaro Region*). Utekelezaji wa mradi huu ulijumuisha kufanyika Mdahalo wa kitaifa kuhusu matumizi endelevu ya ardhi ulioshirikisha wadau **102**; kutoa mafunzo ya kuwezesha vikundi vya jamii kuwa na hadhi ya kisheria na kuweza kukubalika na taasisi za fedha kwa ajili ya mikopo; Kaya **224** zilifunzwa kuhusu namna ya kunufaika na biashara ya hewa ukaa na utengenezaji wa majiko banifu; na Mafunzo kwa kaya **300** na taasisi **200** kuhusu matumizi sahihi ya kuni na mkaa yalitolewa. Aidha, shughuli nyengine zilizotekelezwa ni pamoja na; Ujenzi wa Matenki ya maji katika vijiji, uchimbaji wa mifereji, Ujenzi wa Makinga maji (*Gabions*) kwa lengo la kupunguza kasi ya maji yanayosababisha mmomonyoko wa udongo; na Kuboresha skimu za asili za umwagiliaji, kama inavyoonekana katika ibara ya 90 ukurasa wa 60-61 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa tatu ni ule wa Kuhuisha Masuala ya Usimamizi Endelevu wa Misitu ya Miombo katika Mikoa ya Tabora na Katavi (*Mainstreaming Sustainable Forestry Management in Miombo Woodland Tabora and Katavi*). Shughuli zilizofanyika katika kipindi hiki ni pamoja na kusambaza mizinga ya nyuki **120** kwa wanavijiji katika maeneo ya mradi na kutoa mafunzo ya kilimo na ufugaji wa kisasa wa nyuki na kuku wa kienyeji. Vile vile, Mradi umetoa kiasi cha shilingi **120,000,000/=** kwa SACCOS ya Kijiji cha Mbola katika Wilaya ya Uyui.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli za Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame na miradi inayotekelezwa chini ya Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Usimamizi wa Matumizi ya Mifuko ya Plastiki, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau imeandaa Rasimu ya Kanuni za Plastiki ya mwaka 2013. Rasimu ya Kanuni hii inaendana na viwango vya ubora vya mifuko ya plastiki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyopitishwa mwaka 2012. Rasimu hii itatoa fursa ya kutumika kwa baadhi ya bidhaa za plastiki kwa ajili ya shughuli muhimu katika viwanda vya aina mbalimbali kama vile vya sekta ya maziwa, na usindikaji wa vyakula. Kwa mwaka wa fedha 2014/15 Ofisi itakamilisha Rasimu ya Kanuni na itaendelea kufuatilia utekelezaji wake.

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Baraza liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kuzingatia Sera ya Mazingira ya mwaka 1997, Mpango Mkakati wa Baraza (*NEMC Strategic Plan 2010 - 2014*), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, nyaraka na mikakati mingine ya kitaifa ya kuhifadhi mazingira, kuondoa umaskini na kuleta maendeleo endelevu hapa nchini.

Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira

84. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hiki, Baraza lilifanya ukaguzi wa mazingira katika viwanda na mahoteli ambayo hayajafanya Tathmini ya

Athari kwa Mazingira (TAM) au Ukaguzi wa Awali wa Mazingira (*Initial Environmental Audit*) katika Mikoa ya Mwanza, Morogoro, Dar es Salaam, Mbeya, Tanga, Mtwara, na Lindi kama inavyoonekana katika ukurasa wa 65 hadi 70 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

85. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza lilifanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM), na jumla ya taarifa za TAM za miradi **935** zilifanyiwa mapitio. Miradi **298** kati ya hiyo ilipata Hati za TAM. Aidha, Wataalam **131** na makampuni **32** yalisajiliwa kufanya TAM, na kwa upande wa ukaguzi wa mazingira wataalam **58** na makampuni **16** yalisajiliwa. Miradi **170** ilifanyiwa ufuatiliaji ambapo miradi **14** ni ya uchimbaji wa madini na miradi **156** ni ya vituo vya mafuta. Vilevile, ufuatiliaji ulifanyika kwa wawekezaji **47** wenye leseni za uchimbaji madini na kuagizwa kufanya ukaguzi wa mazingira (*Environmental Audit*) kwa shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Kuhifadhi Mazingira kwa Umma kupitia Baraza la Hifadhi ya Mazingira imetolewa na kujenga uwezo wa kuhuisha masuala ya mazingira na kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwenye programu na mipango ya maendeleo ya Halmashauri za Wilaya kwa Wakuu wa Idara na Maofisa Waandamizi **180** wa Halmashauri za Wilaya za Iramba, Singida, Ukerewe, Sengerema, Kwimba, Kilwa na Lindi. Hii inafanya jumla ya Wilaya zilizofikiwa na mafunzo haya kufikia **32** tangu mradi ulipoanza mwaka 2012.

86. Baraza pia lilitoa elimu ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa wadau wapatao **80** ambao ni Maofisa wa Polisi, Wanasheria wa Serikali za Mitaa, Mahakimu na wadau wa asasi zisizo za kiserikali katika Mikoa ya Mara, Kigoma, Mtwara na Arusha. Aidha, Baraza limepeleka makala za video zilizoandaliwa katika Wilaya za Dodoma vijijini, Iringa, Meatu, Magu na Bariadi katika vituo vya luninga na radio vilivyopo katika Kanda za Kusini Nyanda za Juu na Kanda ya Ziwa kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi na jinsi ya kuhimili. Baadhi ya

makala hizo zimeanza kurushwa hewani kupitia kituo cha *Iringa Municipal Television (IMTV) na shirika la Taifa la utanganzaji (TBC).*

87. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mkoa wa Iringa, Baraza lilitembelea na kuandaa makala ya filamu inayoonesha athari zinazowakabili na harakati wanazotumia wananchi katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Mto Ruaha, itakayoanza kuoneshwa katika vituo mbalimbali vya televisheni kuanzia mwaka wa fedha ujao. Vilevile, Baraza lilitayarisha na kuchapisha vijitabu **1500** (*policy briefs*) vilivyolenga kuelimisha, kwa lugha nyepesi, kuhusu jinsi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kisera katika sekta za Mifugo, Uvuvi, Bahari na Mazingira ya Pwani. Pia, machapisho ya vibonzo **1,500** vinavyoelezea jinsi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwenye sekta za Mifugo, Misitu, Miundombinu na Makazi ya Binadamu yalisambazwa. Aidha, Kalenda **500** na "*diaries*" **500** za mwaka 2014 zenye ujumbe mbalimbali kuhusu utunzaji mazingira na jinsi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi zilitayarishwa na kusambazwa kwa wadau.

88. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza kupitia ufadhili wa Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP) limeshirikiana na wadau kuandaa *Rasimu ya Mwongozo wa Kutoa Elimu ya Uzalishaji na Matumizi Endelevu ya Rasilimali,* itakayotumiwa na Walimu na Wakufunzi ili kuendeleza matumizi endelevu ya rasilimali. Rasimu hiyo imefanyiwa majaribio katika Kanda za Kati, Nyanda za Juu na Kusini. Kwa sasa Rasimu hiyo inaharirwa ili ichapishwe na kuwa Mwongozo utakaotumika rasmi katika taasisi za elimu kuanzia mwaka wa fedha 2014/15.

89. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2013/14, Baraza limeboresha tovuti yake www.nemc.or.tz kwa kuweka taarifa mpya na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za mazingira. Baraza pia limeendelea kusimamia tovuti ya Taifa ya Mazingira (*Tanzania Environment Web Portal*) iliyozinduliwa mwaka 2012 ikiwa ni mojawapo ya vyanzo vya upatikanaji wa taarifa za mazingira kwa wadau. Aidha, Ofisi ilikamilisha maandalizi ya

mfumo wa kompyuta utakaotunza taarifa zinazohusu mapitio ya ripoti za TAM na Ukaguzi wa Mazingira na kuwezesha wadau kufuatilia habari zinazohusu; mchakato wa tathmini za miradi yao, kujua Wataalamu wa Tathmini za Athari kwa Mazingira *(Environmental Empact Assesment Experts),* Wakaguzi wa Mazingira *(Envvironment Audit Experts)* pamoja na kampuni zilizosajiliwa kwa ajili ya kufanya TAM na Ukaguzi wa Mazingira.

90. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia mradi wa "*Oil for Development"* unaofadhiliwa na Serikali ya Norway, Baraza linashirikiana na Taasisi ya Mazingira ya Norway ili kuboresha mfumo uliopo wa taarifa za kijiografia (*Geographical Information System*). Hatua hii italiongezea Baraza uwezo wa kukusanya, kutunza na kusambaza taarifa za mazingira zikiwemo za utafutaji wa mafuta na gesi asilia pamoja na taarifa za uchimbaji wa gesi asilia unaoendelea.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, Baraza litaendelea kukusanya taarifa na kutoa elimu ya mazingira kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira katika maeneo makubwa matano ambayo ni:- Kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; Masuala ya mazingira katika sekta mpya za gesi na uchimbaji wa madini ya urani; Matumizi endelevu ya rasilimali za nchi; Namna ya kudhibiti utupaji ovyo wa taka; na Udhibiti wa ujenzi holela katika fukwe za mito, bahari, maziwa, mabonde na vyanzo vya maji. Baraza litaendelea pia kusambaza makala za video katika vituo vya luninga na radio vilivyopo katika Kanda zingine ili kukuza uelewa wa jamii kuhusu athari na jinsi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Mipango ya Mazingira na Utafiti wa Mazingira

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14, Baraza limekusanya taarifa za hali ya mazingira katika maeneo ya pwani na milima na kufanya ukaguzi wa awali katika Mto Mkundi uliopo Morogoro na eneo la dakio (*catchment area*) mwezi Machi, 2014 na kubaini uharibifu

uliosababishwa na mafuriko. Taarifa ya awali imeandaliwa ikitoa mapendekezo ya kurekebisha na kuzuia madhara kutokea tena. Vilevile, Baraza lilikamilisha taarifa za hali ya milima katika mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, Baraza litaendelea kutekeleza Agenda ya Taifa ya Utafiti Katika Mazingira (*National Environmental Research Agenda - NERA)*; Kupanga mipango ya hifadhi ya mazingira katika maeneo maalum; Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa hali ya mazingira katika mifumo ikolojia; na kuwezesha utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa hifadhi ya mazingira katika ngazi za wilaya na vijiji.

Ujenzi wa Jengo la Baraza (*Mazingira House*)

94. ***Mheshimiwa Spika,*** juhudi za kutekeleza mpango wa ujenzi wa Ofisi ya Baraza katika eneo la Mikocheni, Mtaa wa Regency/Migombani ziliendelezwa kwa kununua Kiwanja Na. **28** kinachopakana na Viwanja Na. **29** na **30** vilivyopo katika eneo la Ofisi za Baraza, ili kupata eneo la kutosha linalokidhi mahitaji ya ujenzi huo. Michoro ya jengo hilo inaandaliwa na jitihada za kutafuta fedha zinafanywa tukiwa na matumaini ya kuanza ujenzi ndani ya mwaka wa fedha 2014/15.

Ukusanyaji wa Tozo za Mazingira

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14, Baraza lilikadiria kukusanya tozo kiasi cha shilingi **1,500,000,000/=** hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 kiasi cha shilingi **856,000,000/=** zilikuwa zimekusanywa, sawa na asilimia **58** ya makadirio. Kutofikiwa malengo ya ukusanyaji kunatokana na uwezo mdogo wa Baraza kifedha na upungufu wa vitendea kazi; ufahamu mdogo kuhusu Kanuni za Tozo za mwaka **2008** pamoja na Sheria ya Mazingira ya Sura **191** kwa wamiliki wa viwanda na wawekezaji. Katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Baraza litaendelea

kutafuta vyanzo vipya vya fedha na kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na tozo za mazingira.

Uratibu wa Miradi ya Kusimamia na Kuhifadhi Mazingira

96. ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi iliyosimamiwa katika programu hii ni; Mosi, Mradi wa Binadamu na Mazingira Hai (*Man and Biosphere Reserves – MAB*), unaowajengea uwezo wadau walioko pembezoni mwa Hifadhi Hai ya Milima ya Usambara Mashariki ili waweze kuibua na kuanzisha shughuli za kipato ambazo ni rafiki kwa mazingira. Pili, Mradi wa "*Oil for Development"* Tatu, mradi wa kuhuisha masuala ya Mazingira na Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi unaotekelezwa kwa muda wa miaka minne **(4)** (2012/13 – 2014/15) na kufadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa. Miradi hii inalenga kujenga uwezo wa wananchi kufahamu chanzo, athari na jinsi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, Baraza limetoa mafunzo ya uhifadhi wa mazingira kwa wajasiriamali na waendelezaji wa miradi ya nishati (*local entreprenuers)* na Washirika wao, maafisa mazingira wa Halmashauri na manispaa katika Mikoa ya Njombe, Katavi na Rukwa. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria ya usimamizi wa Mazingira katika uendelezaji wa miradi ya nishati hususan nishati jadidifu (*pico, micro na small hydro, solar*, upepo na tungamotaka (*biomass*) umefanyika katika Mikoa hiyo;

98. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, Baraza litaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo na kubuni miradi mingine mipya.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeanza utekelezaji wa Mradi wa Kuhifadhi Bonde la Kihansi pamoja na lindimaji (*Kihansi Catchment*

Conservation Management Project) kwa kupitisha Mpango Kazi wa Mradi. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano **(5)** kwa ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Mazingira. Utekelezaji wa Mradi huu umegawanyika katika vipengele vikuu viwili ambavyo ni kujenga uwezo wa kitaasisi katika usimamizi wa Bonde la Kihansi na kutunza viumbe ndwele vilivyopo katika Bonde hilo.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojkitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano, na Usimamizi na hifadhi ya mazingira ni pamoja na; upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Ofisi, jamii kuwa na uelewa mdogo kuhusu masuala ya muungano na masuala ya mazingira, mapungufu katika kuwepo na kupatikana kwa wakati takwimu sahihi za mazingira, na mwitikio usioridhisha kwa serikali za Mitaa katika masuala ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua zilizochukuliwa katika kukabiliana na changamoto hizo ni kutafuta fedha za ndani, na kutoka kwa wafadhili, kwa njia ya kuandaa miradi ili kuiwezesha Ofisi kuendelea kutoa elimu kwa umma kupitia redio, luninga, magazeti, machapisho, maadhimisho na maonesho ya kitaifa kuhusu masuala ya Mazingira na Muungano; Kuboresha ukusanyaji wa takwimu kwa kutoa mafunzo na vifaa kwa Waratibu wa Mazingira wa sekta na Maafisa Mazingira wa Serikali za Mitaa; na Kuendelea kuhamasisha Serikali za Mitaa kuhuisha masuala ya mazingira katika mipango yao ya maendeleo.

V. MASUALA YA UTAWALA NA MAENDELEO YA WATUMISHI

101. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2013/14, Ofisi pamoja na Baraza la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira, imefanyia kazi kwa uadilifu masuala ya mafunzo, kupanda vyeo, uboreshaji wa mazingira ya utendaji kazi, upimaji wa viwango vya utendaji kazi, maslahi na stahili za

wafanyakazi, na masuala ya afya za wafanyakazi kama inavyoonekana katika ukarasa wa 84 hadi 87 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

VI. SHUKRANI NA HITIMISHO (U.K 88)

102. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wote waliotusaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii. Napenda kuzitaja baadhi ya Nchi na Mashirika ya Kimataifa yafuatayo:- Serikali ya Norway; Serikali ya Marekani; Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (United Nations Development Progamme - UNDP); United Nations Science and Cultural Organization (UNESCO); Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea; Umoja wa Nchi za Ulaya (EU); Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF); Benki ya Dunia; *International Development Agency* (IDA); Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA); Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA); SADC-REEP; *Wildlife Conservation Society* (WCS); *World Wildlife Fund* (WWF); Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO); *Crop Life International* (CLI); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Shirika la Misaada ya Kiufundi la Ujerumani (GiZ); Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE); na Sekta Binafsi. Aidha, napenda nitumie nafasi hii kuwaomba Washirika wa Maendeleo waendelee kushirikiana nasi katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi katika vita dhidi ya umaskini; kuboresha maisha ya kila Mtanzania; kuhifadhi mazingira; na kudumisha Muungano wetu.

VII. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

103. ***Mheshimiwa Spika***, ili Ofisi iweze kutekeleza malengo yaliyoelezwa katika Hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2014/15 kama ifuatavyo:

FUNGU 26: MAKAMU WA RAIS

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi **5,726,000,000/=** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiasi hicho kinajumuisha fedha za Mishahara shilingi **879,540,000/=** na fedha za Matumizi Mengineyo shilingi **4,847,156,000/=.**

FUNGU 31: OFISI YA MAKAMU WA RAIS

105. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2014/15, naomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe shilingi **56,200,719,000/=** fedha za Matumizi ya Kawaida na **6,562,746,000/=** fedha za Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha shilingi **44,039,608,000/=** fedha zitakazopelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; shilingi **3,832,091,000/=** fedha za ruzuku kwa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kiasi kinachosalia

shilingi **6,070,072,000/=** ni fedha za Matumizi ya Kawaida za Idara na Vitengo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa upande wa fedha za Maendeleo zinajumuisha fedha za ndani shilingi **4,500,000,000/=** na fedha za nje shilingi **2,062,746,000/=.**

106. ***Mheshimiwa Spika,*** *naomba kutoa hoja.*